# TNMC Habari

Toleo No. 0022

TOLEO MAALUMU Septemba,2025

HALIUZWI www.tnmc.go.tz @tnmchabari


# Wauguzi, Wakunga Zaidi Ya 2,000 Wala Kiapo Mganga Mkuu Aitaka Jamii Kuwatia Moyo

UK. 3 & 4





## Wauguzi, Wakunga Mkawe Walinzi Wa Afya Za Wananchi -Muuguzi Mkuu Wa Serikali

UK. 4, 5



MAKALA MAALUM

## Lifahamu Tatizo la Afya ya Akili, Dalili zake na namna ya kupata Matibabu.

UK 10, 11



## Viongozi wa TANNA Wakutana Arusha Kujadili Ustawi wa Chama, Wanachama

UK. 7

JARIDA MAALUMU BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

# "Kutoka Dawati la Mhariri Mkuu



Karibu ujisomee Jarida la Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), lililo katika mfumo wa nakala laini, linaloandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania.

Jarida hili linatolewa kila Mwezi likiwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Mawasiliano wenye lengo la kuhabarisha Umma jinsi Baraza linavyotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.

Habari na matukio tuliyokuandalia katika Jarida hili ni yale yanayohusu taaluma ya Uuguzi na Ukunga na Afya kwa ujumla.

Ikumbukwe kuwa, Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania, chini ya Sheria ya Mwaka 2010 ***(The Nursing and Midwifery Act, 2010)*** ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

**Ninakutakia usomaji mwema.**
**Asante sana**

**Bi.Agnes Mtawa**

**Msajili Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania**

## TIMU YA WAHARIRI WA JARIDA

| | |
|---|---|
| Bi. Agnes Mtawa | MWENYEKITI |
| Mwakapiso Ndimmyake | MHARIRI |
| Irene Chilewa | MRATIBU |
| Ezekiel Nyalusi | MSANIFU JARIDA |

# Wauguzi, Wakunga Zaidi Ya 2,000 Wala Kiapo Mganga Mkuu Aitaka Jamii Kuwatia Moyo



*Na Mwandishi Wetu*

Zaidi ya wauguzi na wakunga 2,000 wamekula kiapo cha utumishi bora wenye kuzingatia Sheria, miiko na maadili ya taaluma ya Uuguzi na ukunga katika mahafali ya 14 ya kitaaluma yaliyofanyika Makao Makuu ya nchi Jijini Dodoma mapema tarehe 17.09.2025.

Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Grace Magembe, ambaye alikuwa Mgeni rasmi, katika hotuba yake, ametambua mchango wa wauguzi na wakunga hapa nchini na kuitaka jamii kuthamini kazi za wataaluma hao katika kuihudumia jamii.

***"Watanzania popote wanaponiona na wanaponisikiliza, tuwatie moyo watumishi wa sekta ya afya, tuwaunge mkono ili waendelee kutoa huduma wakiwa na amani na Wale wacheche wanaokosea, sisi kama serikali , kupitia mabaraza ya kitaaluma, tutashughulikanao-***

***Lakini pia sisi wauguzi na wakunga tuliopo hapa, ukiona mwenzako anakosea usikae kimya ukasema shauri yake hapana sio shauri yake, akiharibu yeye tashwira yetu wote imeharibika".*** Alisisitiza Mganga mkuu wa Serikali.



Dkt. Magembe, ameongeza kuwa taaluma ya Uuguzi na Ukunga ndiyo inayoongoza kwa kuwa na watumishi wengi katika sekta ya Afya ambao ni zaidi ya asilimia 60 hivyo, hili ni kundi kubwa linalotegemewa katika sekta ya afya hapa nchini, akawataka wataalamu hao kuhakikisha wanaviishi viapo vyao vya kitaaluma wanapokuwa katika maeneo ya kazi.

***"Nimefuatilia kwa makini kiapo mlichokiapa hii leo, mmesema kuwa nitatunza kwa uthabiti siri nipatazo, ziwe za wagonjwa, familia, au vinginevyo, ambazo nitazifahamu kwa mujibu wa wito wangu, Sasa sitegemei Muuguzi huyu aje atoe siri za wagonjwa, mkaviishi viapo vyenu"*** alisema. Dkt. Magembe.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Prof. Lilian Msele, alibainisha kuwa katika mahafali hayo ya kitaaluma jumla ya wauguzi na wakunga 2,080 walipata sifa ya kusajiliwa baada ya kufaulu mtihani wa Baraza sawa na asilimia 72 ya waliofaulu mtihani, idadi hii ya wauguzi na wakunga imefikisha jumla ya wauguzi na wakunga 56,082 wenye leseni kote nchini.

Mahafali ya 14 ya kitaaluma imefanyika Jijini Dodoma ikitanguliwa na Mtihani wa usajili na leseni kwa lengo la kuhakiki weledi na umahiri katika taaluma ikiwa ni utaratibu wa Baraza la uuguzi na ukunga Tanzania TNMC uliowekwa kwa mujibu wa Sheria ya uuguzi na ukunga ya mwaka 2010 ambapo, wataaluma huapishwa kabla ya kuwapatia leseni zinazowaruhusu kutoa huduma kwa jamii.

## Wauguzi, Wakunga Mkawe Walinzi Wa Afya Za Wananchi-Muuguzi Mkuu Wa Serikali



*Na Ezekiel Nyalusi*

Muuguzi Mkuu wa Serikali ambaye pia ni Mkurugenzi wa huduma za Uuguzi nchini Bi. Ziada Sellah, amewataka wauguzi na wakunga wapya waliaapa kwenye mahafali ya 14 Jijini Dodoma, kutambua kuwa wao ni walinzi wa afya za wananchi.

Hayo ameyasema wakati wa mahafali ya 14 ya kitaaluma yalifanyika katika Jiji la Dodoma tarehe 17.09.2025.

***"Kipekee kabisa niwapongeze kwa kuweza kufaulu mtihani wa usajili na leseni na hatimaye leo hii mtatunukiwa leseni za kitaaluma na leseni hii ni ishara ya imani, kuwa sisi sasa ni walinzi wa afya na kutunza heshima ya kada ya Uuguzi na Ukunga nchini"*** alisema Bi. Ziada.

Pamoja na Kuwataka wauguzi hao wapya kutambua jukumu la kutunza heshima ya kada hiyo, amewataka wauguzi na wakunga wapya kwenda kuleta chachu ya maendeleo katika maeneo ya kazi.

***"Kwetu sisi tunasema huduma na mawasiliano bora kwa mteja lazima iwe huduma staha na madhubuti jambo ambalo naamini hata shule mmesoma, hivyo ni vyema tukatoe huduma bora kwa kujadiliana na wateja kwa lugha zenye staha."*** alisema Bi. Ziada.

Aliongeza kuwa, wauguzi wanapaswa kujiendeleza kitaaluma kwani taaluma ya Uuguzi na Ukunga inakua kila uchwao hivyo itasaidia kuendana na kasi ya mabadiliko ya kisayansi na teknolojia.

# Wauguzi, Wakunga KCMC Wakumbushana Umuhimu wa Kuhuisha Leseni Za Kitaaluma

*Na Mwandishi Wetu*

Chama cha Wauguzi na Wakunga Tanzania (TANNA) Tawi la KCMC kimefanya mkutano wake wa robo mwaka uliowakutanisha wanachama wake wanaofanya kazi kama wauguzi na wakunga katika hospitali hiyo Miongoni mwa masuala muhimu yaliyojadiliwa ni kuwakumbusha Wauguzi na wakunga umuhimu wa kuhuisha leseni zao za kitaaluma.

Akizungumza na wataaluma hao Mkurugenzi wa huduma za uuguzi na ukunga katika Taasisi hiyo ya afya Bi. Brenda Kitali, amewakumbusha wauguzi na wakunga juu ya uhuishaji wa leseni za kitaaluma kwa muda muafaka ili kutimiza takwa la kisheria ambalo linamtaka kila muuguzi na Mkunga kuwa na leseni hai muda wote wa utoaji huduma za afya hapa nchini.

Bi. Kitali pia, ametoa pongezi kwa watendaji hao kwa umahiri wao wa utoaji huduma hospitalini hapo huku akiwataka kuongeza bidii katika utoaji huduma bora,





zenye staha, kwa kuzingatia maadili, taratibu, kanuni na miongozo ya kitaaluma.

Aidha, sanjari na msisitizo wa kuhuisha leseni na kufanya kazi kwa weledi, mkutano huo pia uliangazia masuala mbalimbali yahusuyo ustawi wa chama na namna ya kuboresha utoaji wa huduma za uuguzi na ukunga katika Hospitali ya KCMC.



# Chuo cha Uuguzi IAMBI Chahimiza Wanafunzi wake Kukamilisha Usajili wa Awali (Student Indexing)

*Na Ezekiel Nyalusi*

Uongozi wa Chuo cha Uuguzi na Ukunga IAMBI kilichopo Mkalama Mkoani Singida, kimechapisha taarifa maalumu kwenye ukurasa wao wa Instagram inayowataka wanafunzi wa kada ya Uuguzi chuoni hapo kuhakikisha wanakamilisha usajili wa awali *(student Indexing)* kabla dirisha maalum la maombi halijafungwa mapema Oktoba 06.2025



## TAARIFA KWA WANAFUNZI WOTE

"kila mwanafunzi anaesoma Astashahada au Stashahada ya Uuguzi na Ukunga ahakikishe swala la *Student indexing* amelifanyia kazi kwa kuzingatia taratibu zote kuanzia passport na mambo mengine yote, Unaweza kupitia kwenye kurasa ya TNMC usome maelekezo, taratibu na jinsi ya kufanya Student indexing ili ukamilishe ipasavyo.

Student indexing inakuwezesha wewe kutambuliwa na TNMC, namaanisha kuwa, TNMC wataona kama unasifa ya kuwa muuguzi namkunga au huna vigezo/kigezo fulani Kupitia huo mfumo ndo utakuwezesha uruhusiwe kufanya mtihani wa leseni ili utambuliwe na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC)

Utaratibu inabidi ujiunge kwenye mfumo wa *STUDENT INDEXING* immediately ukijiunga na chuo ukiwa mwaka wa kwanza  ili ujisajili kama unavigezo utakubaliwa ila kama huna kigezo utakataliwa

Usijeshangaa unamaliza chuo ukiwa na Astashahada/Stashahada ya Uuguzi na Ukunga *(Certificate/Diploma of nursing and midwifery)* alafu unakataliwa kuwa huna sifa ya kuwa Muuguzi na Mkunga wala huruhusiwi kufanya mtihani wa leseni kwa sababu fulani maana mitaala, sifa, vigezo na taratibu zinabadilika kadri mda unavyoenda

Jana katika kikao na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) wamesisitiza kila mwanafunzi afanye *STUDENT INDEXING* na dirisha lipo wazi tangu juzi dirisha limefunguliwa siku 14 hivyo fanyia kazi hili jambo na likifungwa dirisha basi utakuwa *responsible accordingly"*

Baraza la Uuguzi na Ukunga (TNMC) Kupitia Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Bw.Ndimmyake Mwakapiso, wanakipongeza Chuo cha IAMBI kwa kuwa mstari wa mbele kuhamasisha wanafunzi wao kuheshimu na kutekeleza taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa kanuni za udahili wa wanafunzi wanaojiunga na taaluma za uuguzi na ukunga nchini kwani hamasa hii inalenga kuwanusuru wanafunzi hao na hatari ya kutosajiliwa na Baraza mara baada ya kuhitimu masomo yao vyuoni.

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za uuguzi na ukunga Tanzania, chini ya Sheria ya Mwaka 2010 *(The Nursing and Midwifery Act, 2010)* ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

## Viongozi wa TANNA Wakutana Arusha Kujadili Ustawi wa Chama, Wanachama



*Na Mwandishi Wetu*

Kamati Kuu ya Chama cha wauguzi Tanzania (TANNA) kimeketi kwa siku tatu jijini Arusha kuanzia tarehe 24-26 Septemba 2025 kwa lengo la kujadili Ustawi wa chama pamoja na wanataluuma wa kada ya Uuguzi hapa nchini.

Akizungumza na TNMC Habari Katibu Mwenezi wa chama Bw. Prosper Protas, amebainisha kuwa kikao hicho cha kamati kuu hufanyika kwa mujibu wa katiba ya chama na kuangazia masuala mbalimbali yahusuyo chama na wataaluma kwa ujumla

Aidha, kikao hicho kimeongozwa na Mweyekiti TANNA Taifa muuguzi mbobezi Dkt. Ezekiel Mbao, ambaye ni rais wa chama huku wajumbe wengine wakiwa ni Makamu wa rais Bi. Pendo Shayo, Katibu Mkuu Bw. Chacha John, Makamu Katibu Bw. Meshack Makojijo, Mweka Hazina Bi. Emilia Mwakanyanga, Makamu Mweka Hazina, Bw. Yohani Martin, Katibu Mwenezi Bw. Prosper Protas na Makamu Mwenezi Bi. Maria Mtweve.

### TANNA NI NINI NA WAJIBU WAKE KWA WAUGUZI NI UPI?

Chama cha Wauguzi Tanzania, *"Tanzania National Nurses Association"* (TANNA) ni chama cha kitaaluma cha Wauguzi nchini, kilichoanzishwa mwaka 1972 chini ya sheria ya uanzishwaji vyama vya kijamii *"societies ordinance act, 1954 (rule 5)".* Moja ya lengo la chama ni kutetea maslahi ya wauguzi na kuhamasisha wajibu na haki ya Muuguzi katika utoaji wa huduma bora za afya pamoja na kuhakikisha wanataaluma wanatoa huduma bora inayotarajiwa na wateja wetu kwa kuzingatia weledi na miongozo iliyowekwa na kuimarisha ubora wa huduma za Uuguzi kwa kuhamasisha sera bora zinazolenga kuboresha huduma za afya.

# Mimi tayari nime **Subscribe** unasubiri nini?




Muda ni Sasa! Pata taarifa, Makala na Vipindi mbalimbali kuhusu **Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC)**

# KM Shekalaghe, Ahimiza Umoja, Mshikamano Kazini Kwa Watumishi Wizara Ya Afya



Na Mwandishi Wetu

Katibu Mkuu wa Wizara ya afya, Dkt. Seif Shekalaghe, amewahimiza watumishi wa wizara hiyo kuimarisha umoja na mshikamano miongoni mwao, ili kuleta tija na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma bora za Afya kwa wananchi.

Akizungumza katika kikao maalum na watumishi wa Wizara ya afya  Septemba 25, 2025 Mtumba Jijini Dodoma, Katibu Mkuu Dkt. Shekalange amesema, mshikamano kazini ni nguzo muhimu inayowezesha utoaji wa huduma zenye tija kwa wananchi, huku akihimiza kila Mtumishi anapaswa kutimiza wajibu wake kwa weledi, nidhamu na maarifa ili kufikia malengo ya Wizara.



***"Katika utendaji wetu hakuna kada iliyo muhimu kuliko nyingine, leo hii mtu wa masijala asipo sogeza jalada kwa wakati anaweza kuchelewesha huduma kwa mtu aliyepaswa kupewa rufaa kwenda kwenye matibabu, hivyo hata hawa wenzetu wa masijala nao ni matabibu, lakini pia kwa dereva hivyo hivyo na hata kwa mhudumu anayetayarisha chai ya Ofisi, ni rai yangu tuishi kwa kuheshimiana kila mmoja wetu kwa nafasi yake."*** amesema Dkt. Shekalaghe

Dkt. Shekalange ametumia fursa hiyo kutoa shukrani kwa Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa Fedha zilizowezesha kukamilika kwa jengo jipya la Wizara ya afya na kuanza kutumika, huku likitarajiwa kukabidhiwa rasmi mwezi Oktoba mwaka huu.

***"Wengi mnafahamu kuhamia haikuwa kazi rahisi, kwani sisi tulikuwa asilimia 96, tukafanya maamuzi magumu ya kuhamia, ile hali ya kutawanyika kwa ofisi ilikuwa inaturudisha nyuma umoja wetu, lakini sasa tunajuana kwa sababu tupo eneo moja, hizi ni jitihada za Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa Fedha na jengo kukamilika,"*** amesisitiza Dkt. Shekalange.

Aidha, amewataka watumishi kutoa huduma kwa upole na heshima kwa wananchi, kushirikiana wakati wa matatizo, kusaidiana katika changamoto na kuongeza upendo kazini kwa maendeleo ya pamoja, huku akiwasihi wakurugenzi kuwa karibu na watumishi wao, kusikiliza changamoto zao na kuweka mazingira rafiki ya kazi ili kuongeza tija na morali.

# Lifahamu Tatizo la Afya Ya Akili

*Na Mwandishi Wetu*

## AFYA YA AKILI NI NINI?

Ni hali ya mtu kuwa na uwezo wa kufikiri vizuri, kuhisi vizuri,(Mawazo Chanya) kuweza kutimiza majukumu yake ya kila siku kuishi kwa amani na watu wengine.

## SIFA ZA MTU MWENYE AFYA YA AKILI;

1. Anaweza kukubaliana na changamoto za kila siku za maisha
2. Kufanya kazi na shughuli zake vizuri
3. Kufurahia maisha na kuona maisha yanadhamani
4. Kutoa mchango mzuri katika jamii
5. Kudhibiti hisia kama furaha, hasira, huzuni, hofu na msongo wa Mawazo

## CHANGAMOTO YA AFYA YA AKILI

Ni nini maana ya changamoto ya afya ya Akili?

Ni hali ambayo inamfanya mtu kushindwa kufikiri vema, kuhisi (mara nyingi anakuwa na hisia hasi) kushindwa kutekeleza majukumu yake kushindwa kuelewana na jamii inayomzunguka au Kutenda mambo kinyume na Sheria na kanuni zilizopangwa katika jamii husika.

Ni pale ambapo mtu anakumbwa na matatizo ya kihisia, kiakili, au kitabia, ambayo yanaathiri maisha yake ya kila siku.

## MIFANO YA CHANGAMOTO YA AFYA YA AKILI

1. Msongo mkali wa Mawazo (Stress)
2. Huzuni ya muda mrefu (depression)
3. Wasiwasi kupita kiasi (Anxiety)
4. Kuona vitu watu wengine hawavioni



Pamoja na kusikia sauti ambazo watu wengine hawasikii (Hallucination)
5. Hofu ya kushirikiana na watu(Social Anxiety)
6. Kujitenga(Self Isolation)

## DALILI ZINAZOWEZA KUONEKANA

1. Kulia au kukasirika bila sababu
2. Kukosa usingizi au usingizi kupita kiasi
3. Kukosa hamu ya kula au kula kupita kiasi
4. Kujitenga na watu
5. Kukata tamaa au mawazo ya kujiua

## MUHIMU KUZINGATIA

Changamoto hizi hazimaanishi mtu ni “mwenda wazimu,” bali ni magonjwa kama yalivyo magonjwa mengine ambayo yanatibika. Mtu akipata msaada mapema, anaweza kupona na kuishi maisha ya kawaida

## JE, NIFANYE NINI NINAPOMUONA MTU MWENYE DALILI HIZI?

Wahi mapema kwenye kituo cha kutolea huduma za afya ya Akili ukutane na mtaalamu wa afya ya Akili.

i.Kuwa na Ratiba ya Kila Siku Kuwa na mpangilio mzuri wa kulala, kula,

kufanya kazi, na kupumzika kunasaidia kupunguza msongo wa mawazo.

ii.Fanya Mazoezi ya Mwili mara kwa mara Kutembea, kukimbia, au hata mazoezi mepesi nyumbani hutoa homoni za furaha (endorphins) zinazopunguza msongo.

iii.Kula chakula bora, Lishe bora (matunda, mboga, nafaka zisizokobolewa) huimarisha mwili na ubongo, na hivyo kusaidia ustawi wa kiakili.

iv. Pata Usingizi wa Kutosha saa zisizopungua 7–9 ya usingizi kila usiku husaidia ubongo kupumzika na kufikiri vizuri.

v. Jifunze Mbinu za Kupunguza Msongo wa Mawazo kama Meditasheni, maombi, kupumua kwa kina, au yoga husaidia sana kutuliza akili.

vi.Jenga Mahusiano bora Kuwa karibu na familia, marafiki, au watu unaowaamini huleta msaada wa kihisia na kupunguza upweke.

viii.Fanya Shughuli Unazozipenda Hobbi kama kusoma, kuchora, kusikiliza muziki, au kupika hutoa furaha na kupunguza msongo.

ix.Omba Msaada Mapema Unapohisi Shida Usisite kuzungumza namshauri, daktari, au mtu wa karibu ukiona dalili za huzuni au msongo. Jitunze Kihisia Jifunze kujisamehe, kupunguza ukosoaji wa nafsi, na kushukuru mambo madogo ya maisha (gratitude).

***FIKIRI AFYA FIKILI KUCHUA HATUA MARA UONAPO UTOFAUTI WA AFYA YAKO YA AKILI.***

***Makala Hii imeandaliwa na:***
***Bi. Rehema Msanjila***
***Afisa Muuguzi -TNMC***

## Wauguzi, Wakunga wa Jiji la Dodoma Waadhimisha Siku ya Wauguzi, DC Shekimweri Amwaga Sifa

Sherehe ya Maadhimisho ya Siku ya Wauguzi na Wakunga wanaofanyakazi katika Jiji la Dodoma zimefanyika Jijini humo kwa kutoa huduma mbalimbali za afya ikiwa ni sehemu ya shughuli muhimu za maadhimisho hayo.

Muuguzi Mkuu wa Jiji la Dodoma, Bi. Situ Muhunzi, amewaambia wanahabari kwamba wauguzi na wakunga ni kada muhimu katika sekta ya afya inayobeba jukumu kubwa la kutoa huduma bora, amesema kuwa kada hiyo ni uti wa mgongo wa mfumo wa afya.

*"Kada hii ni muhimu sana kuliko tunavyofikiria, katika ngazi zote tupo karibu zaidi na wananchi katika kuwapatia huduma huku tukihakikisha usalama wa Mama na mtoto na kutoa huduma za tiba na kinga kwa jamii"* alisema Bi. Muhunzi.



Aliongeza kuwa huduma zilizotolewa leo katika siku ya kwanza zimeonesha ushiriki wa wananchi katika kupata elimu na huduma za afya.

*"Tumehudumia wananchi 201 siku ya leo, huduma za afya zinazopatikana hapa ni pamoja na kupima magonjwa*





***yasiyoambukiza mfano kisukari na Shinikizo la damu tumehudumia wananchi 43, ushauri nasaha na kupima VVU wananchi 77.***

***Kwa upande wa elimu ya huduma za afya ya uzazi na huduma za uzazi wa mpango wananchi 26 wamepata huduma zetu, huku huduma ya uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi na saratani ya matiti wamehudumiwa wananchi 28"*** aliongeza Bi. Muhunzi.

Kwa upande wake Mgeni rasmi katika tukio hilo Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Alhaj Jabir Shekimweri aliwapongeza wauguzi na wakunga kwa kufanya maadhimisho hayo ikiwa ni ishara ya kutambua mchango wao katika sekta ya afya, amesema kuwa Kada ya Uuguzi na Ukunga itabaki kuwa mhimili wa sekta ya afya.

***"Ninyi ni mhimili muhimu sana katika sekta ya afya, mnatoa huduma nzuri kwa wananchi, kwa mantiki hiyo tunawahimiza kuendelea kuwa sehemu ya kuhakikisha afya za wananchi zinakuwa bora kwa kutoa huduma nzuri, mfanye kazi kwa upendo kwasababu ndio taaluma mliyoichagua"*** alisema Mhe. Shekimweri.

Naye, Afisa Muuguzi Msaidizi Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Christopher Tarimo alisema kuwa uwepo wa mgeni rasmi katika sherehe hizo ni heshima kubwa kwa wauguzi na wakunga wa Jiji la Dodoma na chachu ya kuendelea kutimiza wajibu kwa weledi.



**WASILIANA NA TNMC KUPITIA NAMBA HIZI**

**TUPIGIE:**
0262966062
0262966063
0737962691

**WHATSAPP:**
0737962691

# MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA KUHUSU CPD

Je! nikiwa na CPD Point 60 za eneo moja la Mafunzo ambayo yanayopatikana Eneo la kazi (NON-ACCREDITEED CPD) zinatosha kuhuisha Leseni?

**JIBU:** NDIYO ZINATOSHA

Je! nikiwa na CPD Point 60 za eneo moja la Mafunzo yaliyoratibiwa na kupata Ithibati (ACCREDITEED CPD) zinatosha kuhuisha Leseni?

**JIBU:** NDIYO ZINATOSHA

Je! nikiwa na CPD Point 60 za eneo moja la Mafunzo yanayopatikana kwa njia ya Mtandao (ONLINE CPD) zinatosha kuhuisha Leseni?

**JIBU:** HAPANA *(Hapa ni point 12 tu! ambapo mtaaluma alitakiwa kupata alama 4 kwa mwaka)*

***NOTE:*** *Ukichanganya Non Accredited + Accredited + 12 Point za ONLINE =* **60 Point ( Zinakubaliwa)**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA




# UHUISHAJI LESENI NI TAKWA LA KISHERIA KWA MUUGUZI, MKUNGA

## JE! UMEHUISHA LESENI YAKO YA KITAALUMA?

*#Leseni Yangu Ajira Yangu*

# HABARI PICHA MAHAFALI YA 14 YA KITAALUMA- DODOMA


















# HABARI PICHA MAHAFALI YA 14 YA KITAALUMA- DODOMA


















# TANZIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limepokea kwa Masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele ya haki Mwezi SEPTEMBA, 2025, baada ya kumaliza kazi ya hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao Mahali pema Peponi AMENI.



JINA: EDIKEDNESS MAKOBA
KITUO: GEITA RRH
MKOA: GEITA



JINA: MBELEJE CHIMOMO
KITUO:ST. GASPAR - ITIGI
MKOA: SINGIDA

*"Daima **Tutawakumbuka** Wapendwa **Wetu**"*

WAWEZA KUWASILIANA NASI KWA
WhatsApp
0737 96 26 91

Tufuatilie katika

# Mitandao yetu ya Kijamii

@tnmchabari

LIMETOLEWA NA
KITENGO CHA UHUSIANO NA MAWASILIANO
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA
www.tnmc.go.tz